**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI**
*(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)*

Simu: 023 – 2510013,2510031
Nukushi; +023 – 2510031
Baruapepe: ded@masasidc.go.tz
Tovuti: http://www.masasidc.go.tz

S.L.P.60
Masasi
Mtwara
**TANZANIA**

Kumb. Na. MDC/D.30/19/VOL.I/4 Tarehe: 22/11/2021

# TANGAZO LA KAZI

## UTANGULIZI.

Halmashauri za wilaya ya Masasi na Mji wa Masasi kwa kushirikiana na Wilaya ya ENZKREIS ya Nchini UJERUMANI zinatekeleza mradi wa uhifadhi wa Mazingira chini ya programu ya Uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na madadiliko ya Tabia nchi '**Funding Programme for Municipal Climate Protection and Climate Adaptation Projects"(FKKP).** Hivyo basi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi anawatangazia wananchi wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kuleta maombi ya kazi **(Kazi za Mkataba)** kwa nafasi zilizo ainishwa hapo chini.

### 1. AFISA MAZINGIRA (Nafasi 1)

(a). Sifa za Mwombaji

Kuajiriwa wahitimu wenye Stahashada/shahada ya kwanza ya sayansi/sanaa yenye muelekeo wa usimamizi na hifadhi ya mazingira katika moja ya fani zifuatazo; " Geography and Environmental studies, Aquatic Environmental Science and Conservation, Environmental Science and Management, Environmental Laboratory Science technology, Environmental

Planning and Management" au sifa zinazolingana na hizo kutoka vyuo vinavyo tambulika na serikali.

(b). Kazi za Kufanya.

(i). Kukusanya takwimu na taarifa mbalimbali zinazohusu usimamizi na hifadhi ya mazingira
(ii). Kutoa elimu na mafunzo ya hifadhi ya mazingira kwa wadau mbalimbali
(iii). Kushiriki katika kuandaa mpango wa kazi wa uendeshaji wa shughuli mbalimbali za kituo.
(iv). Kushiriki katika kuandaa na kuendesha maonyesho mbalimbali yatakayo andaliwa na kituo.
(v.) Kufuatilia utekelezaji wa sera na sheria zinazohusiana na usimamizi wa mazingira
(vi.) Kufuatilia na kuainisha maeneo yanayopaswa kuhifadhiwa
(vii. Kuandaa na kutoa taarifa za shughuli mbalimbali za mradi zilizotekelzwa kwa kila mwezi na wakati wowote zinapohitajika.
(viii.) Kufanya kazi nyingine atangazopangiwa kulingana na uwezo na taaluma yake
(ix. kutunza nyaraka na kumbukumbu mbalimbali kituoni.

(c)Mshahara

Kutegemeana na Makubaliano.

(d) Kituo cha Kazi

Kituo cha Elimu na Uhifadhi wa Mazingira (Masasi Mjini)

**2. FUNDI SANIFU (UMEME) – (Nafasi 1)**

(a). Sifa za mwombaji

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha IV/VI na kufuzu mafunzo ya VETA,Astashahada na Stashahada ya Kawaida katika fani ya ufundi wa umeme,Umeme Jua au Mafunzo ya Nishati

Jadididifu**(Renewable Energy)** kutoka chuo kinachotambulika na serikali

(b) Kazi za kufanya.

(i).Kutoa elimu kuhusiana na mifumo ya nishaji Jadididifu kwa wadau mbalimbali kituoni na kwenye eneo la mradi.

(ii). Kuhakikisha kwamba shughuli za matengenezo na ukarabati wa vifaa vya umeme zinatekelezwa kama zilivyopangwa

(iii). Kufanya usanifu na ukarabati wa miradi midogomidogo ya umeme jua iliyopo katika eneo la mradi.

(iv).Kutayarisha mpango mzima na gharama za matengenezo na kushauri uongozi wa juu ipasavyo; kuratibu utekelezaji wa matengenezo, matatizo yanayojitokeza na kushauri uongozi wa juu ili ikibidi kufanya mabadiliko kurahisisha utekelezaji wake.

(vi). Kuongoza watumishi na wanafunzi waliopata mafunzo ya ukarabati wa mitambo ya umeme jua waliopo kwenye eneo la mradi, kufanya matengenezo na ukarabati mara kwa mara.

(vii). Kuandaa na kushiriki katika maonesho mbalimbali yahusuyo nishati jadididifu

(vii). Kutunza vifaa na mitambo yote ya umeme iliyopo kituoni

(viii). Kuandaa taarifa za kila mwezi za shughuli zilizofanyika na kila zitakapohitajika.

(ix) Kufanya shughuli zingine atakazopangiwa.

(d) Kituo cha Kazi

Kituo cha Elimu na Uhifadhi wa Mazingira (Masasi Mjini)

## MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WA NAFASI ZA KAZI

a. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45
b. Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi
c. Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa
d. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, kidato cha nne au cha sita na vyeti vya mafunzo mbalimbali vinavyo husika
e. Waombaji wote waambatanishe picha ndogo mbili (passport size) zilizopigwa hivi karibuni
f. **Testimonials, provisional results, statement of results, result slips havitakubaliwa.**
g. Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne au sita/ cheti cha taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na baraza la mitihani la taifa (NECTA) na baraza la elimu ya ufundi (NACTE)
h. Waombaji Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili
i. Uwasilishaji wa taarifa za kughushi wahusika wataadhibiwa kwa mujibu wa sharia
j. **Muda wa mkataba ni miaka mitatu (3)**
k. Maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza na yawasilishwe kupitia anuani ifuatayo

Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashuri ya Wialaya ya Masasi
S.L.P 60, MASASI – MTWARA

**Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 12/12/2021.**

Limetolewa na;

APOO C. TINDWA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
**MASASI.**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
S. L. P. 60, MASASI